



TAARIFA YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI

TAREHE: OCTOBA 10 2020

MAHALI: ARUSHA, TANZANIA

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)¹ limefikia makubaliano ya awali na Serikali ya Tanzania katika Makubaliano ya Serikali Mwenyeji (HGA) na Mradi wa Bomba la Mafuta.

Hatua hii ya msingi kuelekea utekelezaji wa Mradi wa EACOP ni kielelezo cha mafanikio mengine katika Mchakato, kufuatia Makubaliano ya Awali ya Serikali Mwenyeji upande wa Uganda mnamo tarehe 11 Septemba 2020.

Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli na Mheshimiwa Rais Yoweri Kaguta Museveni wa Jamhuri ya Uganda walikutana Chato, tarehe 13 Septemba 2020, kwa ajili ya makubaliano ya masuala ya pamoja katika Mradi baina ya nchi hizi mbili. Ambapo, walikubaliana kuwa kila nchi kwa uharaka itakamilisha Makubaliano ya Serikali Mwenyeji kwa upande wake na Mradi.

Kila nchi inatakiwa kukamilisha Makubaliano ya Serikali Mwenyeji, yatakayokamilishwa kati ya kila nchi na Mradi wa EACOP ili kuweza kutekeleza Makubaliano kati ya Nchi Mbili Husika kwa ajili ya Mfumo wa Bomba la Mafuta ambao uliidhinishwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda tarehe 25 Mei 2017.

Mwanzoni mwa mwezi Octoba 2020, wawakilishi wa Serikali ya Tanzania na Mradi wa Bomba la Mafuta walikutana mkoani Arusha, kumalizia majadiliano kwa ajili ya Makubaliano na Serikali Mwenyeji kwa upande wa Tanzania ambayo yamejumisha kati ya maswala mengine uidhinishwaji wa Mradi, haki za ardhi, matumizi ya rasilimali za ndani, maswala ya Afya Usalama na Mazingira pamoja na viwango vya ajira.

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) na Serikali ya Tanzania wataendelea kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha mafanikio ya utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kwa kuzingatia Sheria za nchi pamoja na viwango bora vya kimataifa.

Bomba la Mafuta Ghafi litafungua fursa Afrika Mashariki kwa kuvutia wawekezaji. Mradi utapelekea kuwa na ongezeko la zaidi ya asilimia 60% ya Fedha za moja kwa moja za Kigeni (FDI) nchini Uganda na Tanzania katika kipindi cha ujenzi. Msingi wa mafanikio ya Mradi utapatikana kupitia ushirikiano mzuri na uelewano wa wadau wote.

¹ Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki linaundwa na bomba la inchi 24 linalotunza joto na kufunikwa ardhini, vituo sita vya kusukuma mafuta (viwili viko nchini Uganda na vinne viko Tanzania), vituo viwili vya kupunguza kasi ya mafuta vyote viko nchini Tanzania pamoja na Kituo kwa ajili ya usafirishaji wa mafuta kilicho katika eneo la bahari. Mafuta ya Uganda yana asili ya uzito na hali ya nta hivyo kuhitaji mafuta hayo kusafirikwa katika kiwango cha nyuzi joto 50° ili yaweze kufikia kiwango cha kutiririka. Ilikuhakikisha bomba linakuwa na kiwango cha joto kinachohitajika, bomba litapashwa joto kwa njia ya umeme, na kulifanya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kuwa bomba refu zaidi duniani linalopashwa joto kwa njia ya umeme.



-MWISHO-

Kwa taarifa zaidi au kufanya mahojiano kwa ajili ya vyombo vya habari tafadhali wasiliana nasi kupitia:

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano,
Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi – Tanzania
Mariagoreth Charles

Simu ya ofisi: +255 22 2214100/4102/4103
Simu ya mkononi: +255 699 000 341
Baruapepe: mariagoreth.muangirwa@external.total.com
Tovuti: www.eacop.com